# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 998

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-771-5

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III - VI nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA SANAA NA MICHEZO ELIMU YA MSINGI
# DARASA LA III - VI

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023
Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-771-5

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama : Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III - VI.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III - VI ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla Elimu ya Msingi Darasa la III - VI ........ 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Elimu ya Msingi Darasa la III - VI ........ 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
7.0 Mbinu Pendekezwa za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ........ 6
10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Umahiri Husika ........ 7
Darasa la III ........ 8
Darasa la IV ........ 13
Darasa la V ........ 19
Darasa la VI ........ 28
Bibliografia ........ 32

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi Darasa la III-VI ........ 3
Jedwali Na. 2: Maudhui ya Darasa la III ........ 8
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa la IV ........ 13
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Darasa la V........ 19
Jedwali Na. 5: Maudhui ya Darasa la VI ........ 28

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III-VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia kazi ya Maboresho ya Mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndiyo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Sanaa na Michezo ni somo la lazima kwa mwanafunzi wa Elimu ya Msingi kuanzia Darasa la III hadi VI. Lengo la kufundisha somo hili ni kumwezesha mwanafunzi kuwa na umahiri katika kubuni kazi za sanaa, kuimarisha afya, kumudu stadi za maonesho ya kazi za sanaa na mashindano ya michezo kwa manufaa binafsi na ya jamii. Mwanafunzi atamudu misingi ya awali ya uimbaji na uigizaji, kuchora picha na kufinyanga maumbo sahili. Vilevile, somo hili litamwezesha mwanafunzi kumudu mazoezi ya viungo, michezo ya asili na michezo ya kisasa pamoja na kushiriki katika maonesho ya kazi za sanaa na michezo katika ngazi ya darasa na shule.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi, Darasa la III-VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Aidha, Muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa III - VI ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kufahamu, kutumia na kuthamini lugha za Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja ya kigeni;
(c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
(d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
(e) Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;
(f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;
(g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;
(h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;
(i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
(j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 4.0 Umahiri wa Jumla Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III - VI ni:

(a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kutumia na kuthamini lugha za Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja ya kigeni;
(c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
(d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
(e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;
(f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali ;
(g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;
(i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
(j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Muhtasari wa somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi kwa Darasa III - VI una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyoonekana katika Jedwali Na 1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi Darasa la III-VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kubuni kazi za sanaa | 1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji<br>1.2 Kuchora picha<br>1.3 Kufinyanga maumbo mbalimbali<br>1.4 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali |
| 2.0 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 2.1 Kumudu mazoezi ya viungo<br>2.2 Kucheza michezo ya asili<br>2.3 Kucheza michezo ya kisasa |
| 3.0 Kumudu kazi za sanaa na michezo | 3.1 Kushiriki maonesho ya kazi za sanaa na michezo |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu hayo ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Sanaa na Michezo;
(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:
    (i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na
    (ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji.
(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Njia za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;
(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;
(e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;
(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;
(g) Kuhakikisha kuwa tendo la ujifunzaji na ufundishaji linafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;
(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;
(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika ukuaji na ujifunzaji wa mwanafunzi; na
(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
(b) Kupata umahiri uliokusudiwa kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa;
(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji; na
(d) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, na machapisho mengine katika maktaba mtandao.

### 6.3 Mzazi/mlezi

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
(b) Pale inapowezekana kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma;
(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;
(d) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mtoto;
(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;
(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na
(g) Kumfundisha mtoto juu ya umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sanaa na Michezo utaongozwa na ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha

mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi. Mbinu hizo ni ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali, majadiliano katika vikundi na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, kazimradi, kazi za vitendo, na kazi nyingine zinazohusiana kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

## 8.0 Zana/vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi zinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea itatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu ufundishaji na ujifunzaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa Somo la Sanaa na Michezo utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kumwezesha mwanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazimradi, mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la

Sita ambao utachangia alama 7.5 katika mtihani wa Kidato cha Nne.

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III - VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi vinne (4) kwa Darasa la III na la IV; na vipindi vitano (5) kwa Darasa la V na VI kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Sanaa na Michezo Elimu ya Msingi Darasa la III - VI umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, vigezo vya upimaji, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vifaa/zana pamoja na idadi ya vipindi kama inavyojitokeza katika Jedwali Na. 2 hadi 5.

## Darasa la III

**Jedwali Na. 2:** *Maudhui ya Darasa la III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kubuni kazi za sanaa | 1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | (a) Kuigiza sauti za viumbe vilivyo hai na visivyo hai | **Fikiri-Andika-Jozisha-Shirikisha:** Waongoze wanafunzi kuigiza sauti za viumbe vilivyo hai na visivyo hai kwa kufikiri, kuandika majina ya viumbe, kujozisha na kushirikisha<br><br>**Ufaraguzi na Maonesho:** Wapange wanafunzi katika makundi ya kujifunza uigizaji wa matukio mafupi mafupi ili kubaini stadi za kutumia mwili, sauti, ufikirifu katika mazingira yao | Stadi za uigizaji wa sauti za viumbe vilivyo hai na visivyo hai zimebainishwa kwa usahihi | Rekodi za sauti za viumbe hai na visivyo hai, barakoa, maleba na matini ya michezo ya kuigiza yanayohusu kuigiza sauti za viumbe hai na visivyo hai | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ujifunzaji rika:** Waongoze wanafunzi katika makundi kuandaa na kuwasilisha igizo | | | |
| | | (b) Kuimba kwa sauti moja (*unison singing*) kwa kuzingatia mkao na upumuaji sahihi (*proper posture and breathing*) | **Nyimbo za hadithi:** Waongoze wanafunzi kuimba nyimbo zinazotokana na hadithi<br><br>**Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuonesha matendo yanayosaidia kudhibiti pumzi wakati wa uimbaji<br><br>**Ujifunzaji rika:** Waongoze wanafunzi kuimbiana nyimbo wazipendazo | Uimbaji wa sauti moja kwa kuzingatia mkao na upumuaji sahihi umefanyika kwa usahihi | Matini za nyimbo fupi zenye sauti moja, nyimbo zilizorekodiwa kwa uimbaji wa sauti moja, ala za muziki, vipaza sauti | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia ala za muziki zinazotumika katika mazingira yake kusindikiza nyimbo fupi | **Udadisi:** Andaa mazingira ya wanafunzi kugusa na kufanya majaribio ya vyombo mbalimbali vya muziki wakiwa wenyewe<br>**Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kutumia ala za muziki zinazotumika katika mazingira yao kusindikiza nyimbo fupi | Ala za muziki zinazotumika kwenye mazingira yake zimetumika kwa usahihi kusindikiza nyimbo fupi | Matini za nyimbo fupi, nyimbo zilizorekodiwa kwa kutumia ala mbalimbali za muziki, ala za muziki zinazopatikana katika mazingira | |
| | 1.2 Kuchora picha | (a) Kuchora picha sahili kwa kutumia penseli | **Maswali na Majibu:** Waongoze wanafunzi kutaja maumbo sahili<br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchora picha zinazoelezea hisia | Uchoraji picha kwa kutumia penseli umefanyika kwa usahihi | Picha za mfano zilizochorwa kwa penseli, matini na maumbo ya vitu mbalimbali yenye maelezo ya namna ya kuchora kwa penseli | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na hali kwa kutumia penseli | | | |
| | 1.3 Kufinyanga maumbo mbalimbali | Kufinyanga maumbo sahili | **Oneshombinu:** Fanya kwa vitendo kuelekeza wanafunzi hatua za kufinyanga maumbo sahili<br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kufinyanga maumbo sahili | Maumbo mbalimbali yamefinyangwa kwa usahihi | Udongo, vifaa vya kutayarishia udongo, vifaa vya kuhifadhia udongo, karatasi, gundi ya maji na matini mbalimbali zinazohusu ufinyanzi | 20 |
| 2.0 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 2.1 Kumudu mazoezi ya viungo | Kufanya mazoezi ya wepesi na msawazo (*agility and balance*) | **Oneshombinu:** Waoneshe wanafunzi hatua za kufanya mazoezi ya wepesi na msawazo<br>Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya wepesi na msawazo | Mazoezi ya wepesi na msawazo yamefanyika kwa usahihi | Vifaa vya mazoezi (koni, kamba, ubao wa usawazo) | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kucheza michezo ya asili | Kucheza michezo ya rede, kukimbia na chupa kichwani, kukimbia na kijiko | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza michezo ya kukimbia na chupa kichwani na kukimbia na kijiko | Michezo ya rede, kukimbia na chupa kichwani na kukimbia na kijiko imechezwa kwa usahihi | Mpira wa rede, kijiko, limao au yai na chupa | 30 |
| 3.0 Kumudu stadi za maonesho ya kazi za sanaa na michezo | 3.1 Kushiriki katika maonesho ya kazi za sanaa na michezo | (a) Kufanya maonesho ya kazi za sanaa katika ngazi ya darasa | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kushiriki katika maonesho ya kazi za sanaa | Maonesho ya kazi za sanaa yamefanyika kwa usahihi | Video za maigizo ya majukwaani, nyimbo mbalimbali, vifaa vya sanaa | 10 |
| | | (b) Kushiriki katika mashindano ya michezo katika ngazi ya darasa | Kazimradi: Waongoze wanafunzi katika vikundi kushiriki katika mashindano ya michezo | Mashindano ya michezo yamefanyika kwa usahihi | Vifaa vya michezo | 10 |

## Darasa la IV

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Darasa la IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kubuni kazi za sanaa | 1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | (a) Kufanya mazoezi mbalimbali ya mwili kwa kuigiza viumbe hai na visivyo hai | **Oneshombinu:** Waoneshe wanafunzi hatua za kufanya mazoezi mbalimbali ya mwili kwa kuigiza viumbe hai na visivyo hai<br><br>**Igizodhima:** Waongoze wanafunzi katika kufikiri na kujenga picha za aina mbalimbali za viumbe hai na visivyo hai katika mazingira yao, na kisha kuigiza sauti na matendo yao mbele ya wanafunzi wenzao | Mazoezi mbalimbali ya mwili kwa kuigiza viumbe hai na visivyo hai yamefanyika kwa usahihi | Barakoa, ngoma, maleba, mapambo na vifaa mbalimbali vya kuigizia | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuimba kwa sauti moja na sauti mbili kwa kuzingatia matamshi (*diction*) na toni (*tone*) | **Kufuatisha:** Waongoze wanafunzi kufuatisha namna ya kuimba kwa kuzingatia matamshi na toni<br>**Kutunga nyimbo:** Waongoze wanafunzi kuimbiana nyimbo za kusibu<br>**Hadithi:** Wahusishe wanafunzi katika simulizi zinazotumia nyimbo mbalimbali kwa kuzingatia matamshi na toni<br>**Igizodhima:** Wahusishe wanafunzi katika kuimba nyimbo mbalimbali za uhusika wakizingatia matamshi na toni | Uimbaji kwa sauti moja na sauti mbili kwa kuzingatia matamshi (*diction*) na toni (*tone*) umefanyika kwa usahihi | Matini za nyimbo fupi zenye sauti mbili, nyimbo zilizorekodiwa na ala za muziki | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia ala za muziki zinazotumika katika mazingira yake kusindikiza wimbo wa shule | **Udadisi:** Andaa mazingira ya wanafunzi kupiga ala za muziki wazipendazo<br><br>**Ujifunzaji rika:** Watie moyo wanafunzi wajifunze wao kwa wao kupiga ala za muziki kwa kusindikiza wimbo wa shule | Ala za muziki zimetumika kwa usahihi kusindikiza wimbo wa shule | Matini ya wimbo wa shule na ala za muziki | |
| | 1.2 Kuchora picha | Kuchora picha za vitu mbalimbali kwa kutumia penseli | **Oneshombinu:** Fanya kwa vitendo kuelekeza wanafunzi hatua za kuchora picha kwa kutumia penseli | Picha zimechorwa kwa usahihi kwa kutumia penseli | Vifaa vya kuchorea, penseli za aina mbalimbali na matini mbalimbali zinazohusu uchoraji wa picha | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchora picha kwa kutumia penseli | | | |
| | 1.3 Kufinyanga maumbo mbalimbali | Kufinyanga mfano wa kitu halisi | **Oneshombinu:** Fanya kwa vitendo kuelekeza wanafunzi hatua za kufinyanga mfano wa kitu halisi<br><br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kufinyanga mfano wa kitu halisi | Mfano wa vitu halisi vimefinyangwa kwa usahihi | Udongo, vifaa vya kutayarishia udongo, vifaa vya kuhifadhia udongo, karatasi, gundi ya maji na matini mbalimbali zinazohusu ufinyanzi | 20 |
| 2.0 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 2.1 Kumudu mazoezi ya viungo | Kufanya mazoezi ya kujenga mawasiliano ya viungo na unyumbufu | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kujenga mawasiliano | Mazoezi ya kujenga mawasiliano ya viungo na unyumbufu | Vifaa vya mazoezi (*Balance pad, balance discs, balance boards* na mkeka) | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (*coordination and flexibility*) | ya viungo na unyumbufu | yamefanyika kwa usahihi | | |
| | 2.2 Kucheza michezo ya asili | Kukimbia kwenye gunia na kukimbiza kuku | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kukimbia kwenye gunia na kukimbiza kuku | Michezo ya kukimbia kwenye gunia na kukimbiza kuku imechezwa kwa usahihi | Gunia, kuku, filimbi, koni/alama | 20 |
| | 2.3 Kucheza michezo ya kisasa | Kucheza sarakasi | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza sarakasi | Michezo ya sarakasi imechezwa kwa usahihi | Vifaa vya sarakasi (mkeka, godoro, *spring floor* na kapeti) | 20 |
| 3.0 Kumudu stadi za maonesho ya kazi za sanaa na michezo | 3.1 Kushiriki katika maonesho ya kazi za sanaa na michezo | (a) Kufanya maonesho ya sanaa katika ngazi ya shule | **Maonesho:** Waongoze wanafunzi kufanya maonesho ya kazi za sanaa shuleni | Maonesho ya kazi za sanaa yamefanyika kwa usahihi | Kazi mbalimbali za sanaa | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kushiriki katika mashindano ya michezo katika ngazi ya shule | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kushiriki katika mashindano ya michezo shuleni | Mashindano ya michezo yamefanyika kwa usahihi | Vifaa vya michezo | 20 |

## Darasa la V

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Darasa la V*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kubuni kazi za sanaa | 1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | (a) Kuigiza kwa kutumia vitendo na sauti na vitendo bila sauti (*mime*) | **Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuigiza kwa kutumia vitendo na sauti<br><br>**Uigizaji bubu** *(Mime and pantomime)***:** Waongoze wanafunzi katika kuigiza vitendo vya viumbe hai na visivyo hai kutumia vitendo bila sauti (mime) kwa kusindikizwa na muziki | Tabia za viumbe hai na visivyo hai zimeigizwa kwa usahihi kwa kutumia vitendo na sauti na vitendo bila sauti | Barakoa, ngoma, maleba, mapambo ya mwilini na zana za kuigizia (*props*) | 30 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuimba kwa kuzingatia mienendo ya muziki (*dynamics*) na uwiano wa sauti (*voice balancing*) | **Kufuatisha:** Waongoze wanafunzi kufuatisha namna ya kuimba kwa kuzingatia mienendo ya muziki na uwiano wa sauti<br>**Uchunguzi:** Wapatie wanafunzi fursa ya kuangalia video na kusikiliza audio za kwaya na vikundi mbalimbali vinavyoimba kwa kuzingatia mienendo na uwiano wa sauti<br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kuimba nyimbo kwa sauti angalau mbili | Mienendo ya muziki (dynamics) na uwiano wa sauti (*voice balancing*) vimezingatiwa katika uimbaji | Chati ya wimbo wa sauti mbili, matini za nyimbo fupi, nyimbo zilizorekodiwa, nyimbo za kizalendo za Kitanzania na ala za muziki | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Hadithi:**<br>Wahusishe wanafunzi katika simulizi zinazotumia nyimbo mbalimbali kwa kuzingatia matamshi na toni<br><br>**Igizodhima:**<br>Wahusishe wanafunzi katika kuimba nyimbo mbalimbali za uhusika wakizingatia matamshi na toni | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia ala za muziki kusindikiza uimbaji wa *solfege* (*d r m f s l t d'*) | **Uchunguzi:** Wapatie wanafunzi fursa ya kuangalia video na kusikiliza audio za vikundi mbalimbali vinavyopiga ala kwa ustadi katika kusindikiza uimbaji wa *solfege*<br>**Ujifunzaji rika:** Wachanganye wanafunzi wenye uwezo tofauti tofauti na wahamasishe kufundishana wao kwa wao kupiga ala za muziki | Ala za muziki zimetumika kwa usahihi kusindikiza uimbaji wa *solfege* (*d r m f s l t d'*) | Chati ya wimbo wa sauti mbili, matini za nyimbo fupi, nyimbo zilizorekodiwa, nyimbo za kizalendo za kitanzania, ala za muziki, projekta, kompyuta na chati za alama za *solfege* | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kufuatisha:** Waongoze wanafunzi katika kupiga ala za muziki kwa kufuata skeli za muziki | | | |
| | 1.2 Kuchora picha | Kuchora picha zinazoonesha hisia na hali kwa kutumia penseli | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubainisha vifaa na vitu vya kuchorea picha za vitu mbalimbali<br>**Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kuonesha njia sahihi ya matumizi ya vifaa katika kuchora picha za vitu mbalimbali | Picha za aina mbalimbali zimebuniwa kwa usahihi | Vifaa vya kuchorea na matini mbalimbali zinazohusu mbinu za uchoraji | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Oneshombinu:** Ongoza wanafunzi katika uchaguzi na matumizi sahihi ya vifaa vya kuchorea picha mbalimbali<br><br>**Maonesho:** Ongoza wanafunzi kuandaa sehemu faafu kwa kutundikia kazi walizotengeneza kwa ajili ya majadiliano ya wanadarasa wote | | | |
| | 1.3 Kufinyanga maumbo mbalimbali | Kufinyanga na kuweka nakshi kwenye maumbo mbalimbali | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadili kuhusu sifa za udongo faafu, maandalizi ya udongo, vifaa na mbinu zitumikazo katika ufinyangaji | Maumbo mbalimbali yamefinyangwa na kuwekewa nakshi kwa usahihi | Vifaa vya kuwekea nakshi, udongo, vifaa vya kuhifadhia udongo, vifaa vya kutayarishia udongo, karatasi, | 25 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na ukaushaji wa maumbo mbalimbali<br><br>**Oneshombinu:** Ongoza wanafunzi kwa kuonesha njia sahihi ya kufinyanga na kutia nakshi maumbo mbalimbali<br><br>**Maonesho:** Ongoza wanafunzi kupanga kazi za sanaa kwa ajili ya majadiliano na kujifunza zaidi | | gundi ya maji na matini mbalimbali zinazohusu ufinyanzi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.4 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali | Kutumia makunzi kutengeneza vitu vyenye maumbo sahili | **Majadiliano:** Ongoza majadiliano ya namna ya kuandaa makunzi, vifaa na mbinu mbalimbali za kutengeneza vitu vyenye maumbo mbalimbali | Vitu vyenye maumbo sahili vimetengenezwa kwa usahihi kwa kutumia makunzi | Makunzi mbalimbali, vifaa vya kutengenezea vitu na matini mbalimbali | 25 |
| 2.0 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 2.1 Kumudu mazoezi ya viungo | Kufanya mazoezi ya kujenga nguvu na kasi (*strength and speed*) | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kufanya mazoezi ya kujenga nguvu na kasi | Mazoezi ya kujenga nguvu na kasi yamefanyika kwa usahihi | Vifaa vya mazoezi (koni, filimbi, viunzi na kamba) | 25 |
| | 2.2 Kucheza michezo ya asili | Kuvuta kamba | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza mchezo wa kuvuta kamba | Mchezo wa kuvuta kamba umechezwa kwa usahihi | Kamba, alama na filimbi | 25 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.3 Kucheza michezo ya kisasa | Kucheza mpira wa miguu na netiboli | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza mpira wa miguu na netiboli | Mpira wa miguu na netiboli zimechezwa kwa usahihi | Mpira, filimbi, kadi, koni na vibendera | 25 |

## Darasa la VI

**Jedwali Na. 5:** *Maudhui ya Darasa la VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kubuni kazi za sanaa | 1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji | (a) Kutumia mbinu mbalimbali za uigizaji | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili jinsi uimbaji na uigizaji unavyofanyika katika jamii<br><br>**Maonesho:** Waongoze wanafunzi katika makundi kuandaa mchezo mfupi wa kuigiza wenye dhima inayotokana na jamii yao. Mchezo uoneshwe mbele ya darasa | Mbinu mbalimbali za uigizaji zimetumika kwa usahihi | Barakoa, ngoma, maleba, mapambo ya mwilini, zana za uigizaji | 25 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kucheza ngoma za asili | **Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi kujadili aina mbalimbali za ngoma za hapa nchini na jinsi uchezaji wake unavyofanyika<br><br>**Maonesho:**<br>Waongoze wanafunzi katika makundi kuandaa na kucheza ngoma. Ngoma ibebe ujumbe wowote kutoka katika jamii husika na ichezwe mbele ya wanafunzi wote shuleni | Mbinu mbalimbali za kucheza ngoma zimetumika kwa usahihi | Ngoma, manyanga, njuga, maleba, mapambo ya mwilini, zana za kuchezea ngoma | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuchora picha | Kuchora picha kwa kuangalia vitu mbalimbali | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili kanuni za msingi za kuzingatia wakati wa kuchora picha kwa kuangalia vitu na maumbo mbalimbali halisi<br>**Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kuonesha njia sahihi za kutumia vifaa na mbinu za kuchora picha na vitu halisi kwa kuviangalia.<br>**Maonesho:** Ongoza wanafunzi kupanga kazi za sanaa kwa ajili ya majadiliano ili kujifunza zaidi | Picha zimechorwa kwa usahihi kwa kuangalia na vitu mbalimbali | Vifaa vya kuchorea na kupakia rangi, rangi za maji, maumbo na matini mbalimbali zinazohusu uchoraji | 25 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 2.1 Kumudu mazoezi ya viungo | Kufanya mazoezi ya ustahimilivu (*endurance*) | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya ustahimilivu | Mazoezi ya ustahimilivu yamefanyika kwa usahihi | Vifaa vya mazoezi (kamba ya kuruka, *trade mill,* saa ya michezo) | 25 |
| | 2.2 Kucheza michezo ya asili | Kucheza michezo ya kuruka ya chini na juu | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza michezo ya kuruka chini na juu | Michezo ya kuruka chini na juu imechezwa kwa usahihi | Uwanja wa kurukia, futikamba, nguo za michezo, filimbi, vibendera, saa ya michezo, kibao cha kurukia, kihunzi, godoro | 25 |
| | 2.3 Kucheza michezo mikubwa | Kucheza michezo ya kukimbia | **Mazoezi yanayoratibiwa:** Waongoze wanafunzi kucheza michezo ya kukimbia | Michezo ya kukimbia imechezwa kwa usahihi | Eneo la kukimbilia, filimbi, vibendera, saa ya michezo, kamba, chokaa, nguo za michezo | 25 |

## Bibliografia


Basic Education Department. (2011). *Curriculum and assessment policy statement grades r-3 life skills.* Republic of South Africa.

Boal, A. (2005). *Games for actors and non-actors* (2nd Ed.). Routledge.

Body of Studies New South Wales. (2006). *Creative arts K-6*. Body of Studies New South Wales.

Cambridge Assessment International Education. (2019). *Cambridge primary art & design: Curriculum outline.* Cambridgeinternational.org/

Cambridge Assessment International Education. (2008). *Curriculum framework Cambridge primary physical education 0069.* Cambridge Pathway

Cambridge Assessment International Education. (2008). *Music 0410 for examination in June and November 2020, 2021 and 2022.* Cambridge Pathway.

Cambridge Assessment International Education. (2019). *Syllabus Cambridge IGCSE physical education 0413.* Cambridge Pathway.

Cambridge Assessment International Education. (2019). *Syllabus Cambridge IGCSE drama 0411 version 2*. Cambridge Pathway.

Cambridge Assessment International Education. 0400. (2019). *Cambridge primary art & design:* Curriculum Outline. Cambridge Pathway.

Commonwealth of Virginia Department of Education. (2015). *Sample music curriculum for Virginia public schools:Kindergarten – Grade Twelve*. Virginia Department of Education.

Daubney, A., & Fautley, M. (2019). ISM- *The national Curriculum for Music: A revised pedagogy and assessment across primary music*. Incorporated Society of Musicians.

Gozzoli, C., Locatel, E., Massin, D., Wangemann, B. (2002). *Kids' athletics* (1st Ed*.)*. International Association of Athletics Federations.

Michigan Department of Education. (2011). *Michigan merit curriculum. Standards, benchmarks, and grade level content expectations:* Visual Arts, Music, Dance and Theatre. Vol. 6. Michigan Department of Education.

Ministry of Education Singapore. (2016). *Physical education teaching & learning syllabus primary, secondary & pre-university*. Student Development Curriculum Division.

National Council of Educational Research and Training. (2008). *Syllabus of arts education.* Sri Aurobindo Marg.

National Institute of Education (Maldives). (2015). *Creative arts in the national curriculum*. Key Stage 2 (Grade: 4, 5 and 6). National Curriculum.

Rwanda Academy of Language and Culture. (2019). *Marketing strategies for the promotion of cultural and creative industries in Rwanda*. RALC.

Rwanda Education Board. (2015*). Physical education and sports syllabus upper primary level*. REB.

Stanislavski, Constantin. (2003). *An actor prepares*. Routledge.

Tanner, Fran Averett. (1995). *Basic drama projects sixth edition.* Clark Publishing.

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. (2018). *Michezo na sanaa:* Kitabu cha Mwalimu Darasa la pili. Taasisi ya Elimu Tanzania

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. (2019). *Muhstasari wa somo la maarifa ya jamii elimu ya msingi darasa la III-VI.*

Taasisi ya Elimu Tanzania.